THE WORLD BANK
IBRD • IDA | WORLD BANK GROUP

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Kukuza Maendeleo Endelevu katika Juhudi za Kenya Kuingia Kitengo cha Juu cha Mataifa yenye Mapato ya Wastani

WASHINGTON, Novemba 22, 2022 — Bodi ya wakurugenzi wakuu wa Benki ya Dunia (WBG) leo imeunga mkono mpango wa miaka sita wa Benki ya Dunia kuunga mkono Kenya katika azma yake ya kuendeleza aina ya maendeleo yanayozingatia utunzaji mazingira na yanayohusisha wote.

Mwongozo wa Ushirikiano wa Taifa la Kenya (CPF) unahusu mikakati ya pamoja kati ya Benki ya Dunia (WBG), Shirika la Fedha (IFC) na Shirikisho la Kudhamini Uwekezaji Kimataifa (MIGA) kwa upande mmoja na serikali ya Kenya kwa upande mwingine kwa nia ya kuleta ufanisi wa pamoja na kupunguza viwango vya umaskini kwa Wakenya. Mikakati ya CPF imetokana na mashauriano ya kina kati ya wadau tofauti na inalenga kuboresha utendaji wa wafanyikazi kwa kasi na usawa, kuongeza kiwango cha mapato, kuhimiza usawa katika ugavi wa miradi ya maendeleo na kusaidia Kenya kutunza rasilmali zake asilia ili kudhibiti changamoto zinazotokana na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi.

"Wakenya wana nafasi ya kunufaika zaidi kutokana na kuimarika kwa uchumi wa taifa kwenye suala la kupata suluhu ya kudumu katika kupunguza umaskini*."* Kauli ya **Keith Hansen, Mkurugenzi wa Benki ya Dunia – Kenya**. Keith anaendelea, *"kukabiliana na changamoto zinazoleta ubaguzi kwa sasa, kutasaidia Kenya kuafikia maendeleo zaidi yanayozingatia usawa katika siku zijazo."*

Kwa mwongo mmoja uliopita, uchumi wa Kenya umekua kwa kasi kuliko mataifa mengine yaliyo katika hadhi sawa na Kenya ya kuwa kati ya nchi zilizo kwenye kiwango cha chini na cha kati miongoni mwa mataifa yenye mapato ya wastani (LMIC). Uwepo wa idadi kubwa ya wafanyikazi wenye elimu bora na wenye afya umetajwa kuchangia pakubwa kwa ongezeko la mapato ya Kenya (GDP). Hata hivyo, athari za janga la COVID-19 katika suala la umaskini nchini kumedhihirisha kuwa wananchi wangali kwenye hatari ya kuathirika pakubwa na mikasa. Japo uchumi wa Kenya unazidi kukua kwa kasi baada ya janga la COVID-19 huku ukitarajiwa kukua kwa 5.4% katika kipindi cha 2022-2024, hali ya ukame inayokumba maeneo mengi, mfumko wa bei na kupanda kwa gharama ya maisha inafanya viwango vya umaskini kupanda nchini Kenya. Kwa mujibu wa ushirikiano huu wa CPF, Kenya ingali na nafasi nzuri kukuza uchumi wake kwa namna inayowahusisha wote na Benki ya Dunia iko tayari kutoa msaada unaohitajika haswa katika maeneo ambapo Kenya imezembea kwa nia ya kuzihakikishia jamii zake huduma na miundomisingi bora ili kuziwezesha kujitegemea. Kwa kufanya hivyo, Kenya itasaidika kukwepa mitego inayoyapata mataifa yaliyo katika kitengo cha kati miongoni mwa nchi zenye mapato ya wastani (MIC).

"Sekta ya binafsi nchini Kenya inatarajiwa kuleta ajira zaidi na kuongeza nafasi kutokana na ushirkiano na mataifa katika eneo hili na kimataifa." Kauli ya **Jumoke Jagun-Dokunmu, Mkurugenzi wa IFC - Kenya. Jagun-Dokunmu** anaendelea, "hili litahitaji uwepo wa usawa ili kuzipa biashara ndogo na zile kubwa, za binafsi au umma, fursa sawa ya kupata nafasi zilizopo kulingana na uwezo na ushindani wao*."*

Ushirikiano huu wa CPF unalenga kusaidia kuongeza mapato kwa biashara ndogo, wazalishaji wadogo, wafanyibiashara wa kike, kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini na kuongeza kiwango cha sekta ya binafsi kuhusika katika utoaji wa huduma kwa umma. Ili kusaidia Kenya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na hali ya hewa, ushirikiano huu umeratibu uwekezaji wa aina tofauti ili kusaidia kupunguza tatizo la uhaba wa maji na kuhamasisha kuhusu haja ya kukusanya fedha kushughulikia masuala ya mazingira na hali ya hewa kwa kuwekeza katika sekta za umma na binafsi.

“Shirikisho la Kudhamini Uwekezaji Kimataifa (*MIGA) linalenga kuongeza uwekezaji wa sekta ya binafsi katika miradi inayosaidia kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi na hali ya hewa kupitia kwa mbinu bunifu za ukusanyaji fedha*.” Kauli ya **Merli Baroudi, Mkurugenzi wa Uchumi na Masuala Endelevu - MIGA. Baroudi** anaendelea, **“***ufanisi wa Kenya katika ukusanyaji wa fedha kutoka hazina mbalimbali za binafsi ili kufanikisha mpango wa kuzalisha kawi jadidifu (renewable) umevutia sekta nyingine.***”**

Ushirikiano huu wa CPF umekopa mengi kutoka kwa ruwaza ya Kenya ya 2030, agenda mpya ya serikali kuhusu maendeleo, ripoti ya tathmini ya hali ya taifa, ripoti ya uhakiki wa hali ya sekta ya binafsi nchini, uhakiki wa mikakati ya ushirikiano ya CPF zilizopita na michango ya mashauriano na zaidi ya wadau 34 wakiwepo Wakenya wanaoishi mataifa ya kigeni. Benki ya Dunia ndiye mshirika mkuu wa Kenya katika maendeleo. Kiwango cha IFC kuhusu uwekezaji wa sekta ya binafsi nchini Kenya ndio wa nne katika ukuaji na ndio unaokua kwa kasi zaidi katika eneo la kusini mwa jangwa la Sahara. Wakati huohuo, miradi na mipango ya MIGA nchini Kenya ndiyo ya tatu kwa ukubwa kifedha barani Afrika.

Wasiliana Nasi Kupitia:

Benki ya Dunia: *Vera Rosauer, +254710537030, vrosauer@worldbank.org*
IFC: *Devon Maylie, +1 202 948 6397 (U.S.) | +254112825197 (Kenya), dmaylie@ifc.org*
MIGA: *Elizabeth Howton, +12024585922, ehowton@worldbank.org*

Kwa Maelezo zaidi kuhusu shughuli za Benki ya Dunia nchini Kenya tembelea tovuti hii:
www.worldbank.org/en/kenya/
Kwa Maelezo Zaidi kuhusu IDA, tembelea tovuti hii: www.worldbank.org/ida

Facebook: http://www.facebook.com/worldbankafrica
Twitter: https://twitter.com/worldbankkenya
YouTube: http://www.worldbank.org/africa/youtube

Sikiliza ‘Podcast’ zetu kuhusu masuala ya Uchumi Barani Afrika: https://www.worldbank.org/en/news/series/afronomics-a-podcast-series

Taarifa kwa Vyombo vya Habari
2022/028/AFE